


Pambazuko

Toleo Namba 0039

Jumatatu Mei 22-28, 2023



China yaokoa Mradi wa Eacop

Dkt. Mwinyi aamsha mageuzi

● *Apigania kidemokrasia makini*

Uk. 10-11

JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure

Tahariri

Hongera Rostam kwa uwekezaji Zanzibar

HIVI karibuni Kampuni ya Taifa Energy inayomilikiwa na Mtanzania, Rostam Aziz imepata “baraka” kutoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuwekeza kwenye biashara ya kuzalisha nishati ya umeme wa jua.

Taifa Energy ambayo imeingia ubia na Kampuni ya General Capital Limited (GCL) yenye makao makuu yake nchini Mauritius, imeamua kuwekeza Zanzibar ili kuchochea kasi ya kukua kwa uchumi wa visiwa hivyo kwa kuwa na umeme wa uhakika.

Kampuni hizo mbili zilifunga mkataba wa kuanza mchakato wa kuzalisha nishati hiyo na serikali kupitia Shirika la Umeme la Zanzibar (Zeco).

Mkataba huo umeruhusu kampuni hizo mbili kujenga mtambo wa kuzalisha umeme wa jua na kwamba Zeco ndiyo itakuwa mnunuzi pekee wa nishati hiyo muhimu kuchochea maendeleo.

Mradi huu utachangia megawati 180 kwenye gridi ya taifa.

Pambazuko linampongeza Rostam Aziz pamoja na mshirika wake kwa kuamua kuwekeza Zanzibar, kwani inaonyesha uzalendo wake kwa kuwekeza utajiri wake Tanzania.

Pamoja na kwamba uwekezaji wowote huangalia faida zaidi, ni imani yetu kuwa Rostam, kwa kuwa Mtanzania na mzalendo, hatatumia mwanya wa uwekezaji huo kukandamiza watumiaji wa mwisho wa nishati hiyo ya umeme.

Hapa tunaeleza kwamba imani yetu ni kwamba Rostam, hatauzi

umeme huo kwa Zeco kwa bei za juu, kwani kwa kufanya hivyo, atakuwa anawalazimisha Zeco kuuza nishati hiyo kwa bei za juu zaidi, hatua ambayo tunadhani siyo lengo la serikali wala Rostam.

Tunatambua kwamba ujenzi wa mradi huo mkubwa utakuwa kwa awamu tatu na kuwa ujenzi wa mtambo wa kuzalisha umeme wa jua wa megawati 30 huko Bambi, Wilaya ya Kati Mkoa wa Kusini Unguja.

Kwamba mradi huo utakamilika mwaka 2024 na kugharimu zaidi ya dola za Marekani milioni 140, sawa na shilingi bilioni 330.

Mbali na kuhimiza umeme huo kuuzwa kwa bei ndogo kwa Zeco, Pambazuko linaamini kuwa upembuzi yakinifu umefanyika ili kuhakikisha kuwa mradi huo hauleti madhara katika mazingira.

Dunia hivi sasa iko kwenye mapambano ya kuhakikisha mazingira yanatunzwa ili kuepusha madhara makubwa yanayoweza kutokea na kuvurugwa kwa uoto wa asili, kukatwa kwa miti bila kupanda mingine na shughuli zingine zinazosababishwa na miradi mikubwa.

Ni imani ya Pambazuko kwamba hata kama kutakuwepo na shughuli za kuathiri mazingira, lakini hatua hiyo itafanywa kwa weledi mkubwa kwa kutumia watalaamu wa mazingira na kwamba maeneo ambayo yataguswa - kwa kuvuruga uoto wa asili, lazima yarejeshwe na kutunzwa kwa asili ya mazingira iliyokutwa awali.

Tunamtakia Rostam na mwekezaji mwenzake, mafanikio makubwa katika uwekezaji huo wa nishati ya umeme kwa kutumia jua.

NAWE UTAKUWA RAIS ...



RAIS Samia Suluhu Hassan ampisha mtoto mwenye umri wa miaka minane, Georgina Magesa kwenye kiti chake cha ukuu wa nchi ili kumpa fursa mtoto huyo anayeeleza kuwa na ndoto ya kuwa Rais wa Tanzania. Tukio hilo lilitokea Mei 18, 2023 jijini Dar es Salaam, wakati wa uzinduzi wa minara ya kisasa ya kurusha matangazo ya televisheni ya Azam Media (Picha na Ikulu).

Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: pambazuko1@protonmail.com** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

NUKUU



*“Maisha ni kama kuendesha baiskeli, ili kuendelea mbele, ni lazima kuendelea kukanyaga pedeli kuifanya baiskeli isonge. Ukiacha kukanyaga, siyo tu baiskeli itasimama, bali itaanguka kabisa ” -
Mwanafalsafa Albert Einstein*

Tafakuri

Nasaka duka la kuuza hekima

Na Mwandishi MAALUM

BAADHI ya changamoto zinazolikabili taifa letu kwa sasa zinahitaji hekima kuzitatu. Tatizo hakuna shule wala duka la hekima.

Kinachoonekana kufanyika sasa ni matakwa ya wanasiasa kutumia dhamana zao kufanya uamuzi wa kila jambo, hata ambalo linahitaji zaidi ya kuwahusiana wataalamu wa maeneo husika.

Mengi yameshuhudiwa na wananchi katika siku za hivi karibuni na kubwa ikiwa ni mgogoro kati ya taasisi za serikali na wafanyabiashara wa Kariakoo, Dar es Salaam ambao walifikia hatua ya kuitisha mgomo kwa kufunga maduka yao ili kupaza sauti.

Kilichobainika ni kwamba wapo baadhi ya watendaji wa serikali, hasa taasisi za kukusanya ushuru ambapo ilidhihirika kwamba ziliamua kuchukua uamuzi ambao umeligharimu taifa kwa kiasi kikubwa.

Maswali ni mwengi katika uamuzi wa “wakubwa” hao, lakini itoshe kuuliza haya yafuatayo;

Hivi inakuwaje kiongozi wa serikali anaamua tu kumfilisi mfanyabiashara kwa kumtoa kodi, je, kesho atatoza wapi kodi?

Kwamba mfanyabiashara huyo akitaka asifilisike, anatoa rushwa kwa ofisa wa taasisi na serikali inakosa mapato, huyu ataendelea tu kula rushwa, hivyo kuimarisha msemo kwamba – “Mtoza ushuru hashibi rushwa.”

Huyu mla rushwa, pamoja na kuhatarisha ajira yake kwa kupokea rushwa, hawezi kaucha kwa kuwa amezoea na ataendelea hivyo kwa muda mrefu, labda akamatwe. Huyu atapoteza mapato mengi ya serikali na kuchangia mkwamo wa maendeleo. Je, afanywe nini endapo hatakatika?

Ikiwa ataendelea kwa muda mrefu, huyu mla rushwa, ni dhahiri kwamba ameiba kiasi kikubwa na amechangia kumfilisi; sasa kilichobaki



Wasiri Mkuu Kassim Majaliwa

ni malalamiko kutoka kwa wote; serikali na mfanyabiashara wote wanaungana kumlaumu mtoza ushuru huyu mwizi.

Sasa basi, serikali ikileta mdomo kumtetea mfanyabiashara, inakosa kodi. Ikimtetea mtoza ushuru, biashara zinafungwa. Basi, ni vyema serikali yenye hekima iwekwe mfukoni na wananchi.

Mbali na sakata la Kariakoo, likaibuka jingine, hili ni lile la wafugaji.

Kwamba serikali inamlinda mfugaji dhidi ya mkulima; nchi inakosa chakula.

Kwamba serikali inamlinda mhifadhi dhidi ya mfugaji, nchi inakosa nyama.

Kwamba serikali inaamua kumfilisi mfungaji na kuwatetea ngedere wakati siyo kitoweo.

Wakulima, kama ilivyokuwa kwa wafanyabiashara wa Kariakoo, wanatangaza azma ya kuungana ili waweze kuandamana kwa lengo la kupaza sauti zao zisikike kwa wakubwa na kuchukua hatua.

Hawa wote ni wanyonge ambao wameamua kupigania haki zao kwa kuungana, kuandamana au kuanzisha migomo kwa nia yua “wakubwa” kuwasikiliza na kuchukua hatua stahiki.

Ileleweke kwamba wanyonge wakiungana hakuna wa kuwakwamsha, kwani hufika wakati wakaona hawana chakupoteza.

St Joseph walia kuporomoka maadili

Na Scovya MANASE

WAHITIMU wa kidato cha sita Shule ya St. Joseph Cathedral iliyopo Dar es Salaam wameasa wazazi, walezi wa kiroho na walimu kushirikiana kunusuru kizazi cha vijana kinachopotea kwa kukosa maadili.

Katika risala yao iliyosomwa Jumamosi iliyopita wakati wa mahafali yao, wanafunzi hao walionyeshwa kusikitishwa na kulegalega kwa maadili kwa vijana hatua ambayo walieleza inachangiwa na malezi ya wazazi kwa kutokuwa “karibu” na vijana wao.

Wahitimu hao walieleza kusikitishwa na wazazi wengi kukosa muda wa kufuatilia vyema na kwa karibu makuzi ya vijana wao na hata maendeleo ya kitaaluma ya watoto wao wanapokuwa shuleni au likizo.

“Katika maisha ya sasa wazazi wengi hawana muda wa kufuatilia watoto wao, wanawaacha wafanye na kuenenda wanavyotaka, kiasi cha kuwafanya sasa vijana wengi kuamua kufanya hata mambo yasiyofaa katika jamii,” anasema Daniel Kirigini ambaye ni mmoja wa wahitimu hao 230.

Akitoa nasaha zake katika mahafali hayo, mkuu wa shule hiyo, Sister Theodora Faustine ameeleza kusikitishwa kwake na tabia iliyokomaa katika familia nyingi kwa kuacha vijana wao “kujiongoza” bila mwongozo wa miiko ya familia, taratibu za kaya na jamii.

Sista Theodora anasema vijana katika familia nyingi kwa sasa wanalelewa na vifaa vya kielektroniki, jambo ambalo ni hatari zaidi katika kujenga familia zenye heshima na staha.

“Familia zitalindwa na nani ikiwa jamii itakuwa na vijana ambao wamelelewa na vifaa vya kielektroniki tu! Tunajenga bomu ambalo itakuwa vigumu kulitegua,” akaonya Sista Theodora.

Mkuu huyo wa shule akaeleza pia kwamba kuporomoka kwa maadili ya vijana kunachangiwa na kulegalega kwa



Sista Theodora Faustine

mshikamano na amani ndani ya familia, hasa kwa wazazi.

“Msingi wa malezi bora huanza kwa wazazi, lakini sasa wazazi wengi wamekuwa na uhusiano usioweza kustawisha familia kwa kuwa baba na mama wameshindwa kuelewana, hii huchangia kwa kiasi kikubwa kuparaganyisha maadili ndani ya nyumba na kuwaathiri watoto,” akaongeza.

Mkuu huyo wa shule aliishauri serikali kuangalia namna ya kuwa na sera ama mwongozo ambao utadhibiti matumizi ya simu za mkononi na vifaa vingine vya kielektroniki kwa vijana wadogo ili kuzuia kusambaa kwa tabia zisizoendana na mila na desturi za Tanzania.

Mgeni rasmi katika mahafali hayo, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na wenye Mahitaji Maalum, Dkt. Doroth Gwajima, alisema silaha pekee kwa vijana katika kujilinda na mmomonyoko wa maadili ni kumcha Mungu na kuwasiliza wazazi, walezi na walimu.

“Silaha kubwa kwa vijana ni kuhakikisha maisha yao yanashikamana na mafundisho ya Mungu kwa wanadamu aliowaaumba kwa mfano wake,” aliongeza.

Habari

Mradi wa Eacop wakimbilia China

Na Tryruckia MFINANGA

BAADA ya baadhi ya benki na taasisi za fedha za kimataifa kujitoa kukopesha kiasi kikubwa cha pesa katika kukamilisha ujenzi wa bomba la mafuta kutoka Uganda hadi Tanzania, China imejitosa “kuokoa jahazi.”

Awali, benki na taasisi kadhaa kutoka nchi tajiri za mabara ya Asia, Ulaya na Afrika, zilionyesha nia ya kukopesha mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (Eacop), lakini baadaye zilijitoa kwa madai kwamba mradi huo “haujaweka nguvu kubwa” kulinda na kutetea haki za binadamu na kutunza mazingira.

Mradi huo unaotarajiwa kutumia zaidi dola za Marekani bilioni 3.5, hadi kukamilika kwake, unaelezwa kuwa na upungufu wa dola bilioni 1.8 ambazo hadi wiki iliyopita haikujulikana zitatoka wapi.

Hata hivyo, habari za kuaminika zinaeleza kuwa mkono wa Serikali ya China, umeuhakikishia mradi huo kwamba “itafanikisha” kupatikana kwa kiasi kinachopelea.

Pambazuko limepata taarifa kutoka mji mkuu wa China, Beijing, kwamba uhakika wa kupatikana kwa fedha hizo za mkopo upo na kinachosubiriwa ni Eacop kuwa tayari kuingia mikataba na wakopeshaji hao.

Hata hivyo, benki na taasisi za fedha za China ambazo ziko tayari kuikopesha Eacop hazijawekwa wazi, baada ya kukwama kujibiwa kwa maswali ya Pambazuko yaliyotumwa kwa benkina taasisi kubwa za fedha China kutojibu maswali yaliyotumwa kwao.

Bomba hilo linatoka eneo lenye mafuta huko Kabaale, Hoima nchini Uganda kwenda kwenye peninsula ya Chongoleani mkoani Tanga nchini Tanzania.

Mradi huu una urefu wa jumla ya kilomita 1443 kati ya hizo kilomita 296



Rais Samia Suluhu Hassan sasa anafungua nchi.

zipo nchini Uganda na kilomita 1147 zipo Tanzania. Bomba linapita katika mikoa nane ya Tanzania ambayo ni Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara na Tanga. Bomba vilevile linapita katika wilaya 24, kata 134 na vijiji zaidi ya 180.

Eacop ni miongoni mwa miradi ya kimkakati na mikubwa ambayo inatekelezwa Tanzania.

Mwanahisi mkubwa wa Eacop ni kampuni ya nishati ya TotalEnergies kutoka ya Ufaransa, ambayo ina asilimia 62 ya hisa; Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) ambalo lina asilimia 15 ya hisa; Kampuni ya Taifa ya Mafuta ya Uganda ambayo ina asilimia 15; na Kampuni ya Taifa ya China ya Kuchimba Mafuta (CNOOC), ambayo ina asilimia 8 ya hisa.

Hata hivyo, zipo taarifa kwamba Benki ya Exim ya China ni miongoni mwa taasisi za fedha ambazo zinatajwa kuwa tayari kukopesha fedha kwa mradi huo wa Eacop.

Benki ya Exim ya China ina historia ya kutoa mikopo kwa miradi ya miundombinu ya Uganda.

Mradi wa Eacop wakimbilia China

Inatoka Uk. 6

Pambazuko linaweza kueleza kwamba baadhi ya taasisi za fedha za kimataifa zilizoelezwa kuamua “kujiweka pembeni” kukopesha Eacop ni pamoja na Benki za First Rand na Absa za Afrika Kusini, Allianz ya Australia, Barclays ya Uingereza, Crédit Agricole, Credit Suisse za Ufaransa na Mizuho ya Japan, Munich Re ya Ujerumani, Royal Bank ya Canada na benki za Uswisi; Société Générale, Swiss Re na taasisi zingine.

Pamoja na kuwepo kwa “vizingiti” kutoka kwa mashirika ya kutetea haki za binadamu na ustawi wa mazingira unaodaiwa kukwamishwa na Eacop, serikali za Uganda na Tanzania zimekuwa zikitetea mradi huo kwamba unazingatia kwa kiasi kikubwa utunzaji wa mazingira na kuhakikisha haki za binadamu zinalindwa kwa “kiasi kikubwa.”

Pia wanaharakati wa mazingira wamekuwa wakipinga kuwepo kwa mradi kwamba utavuruga uoto wa asili na hewanga na kushauri wanahisa kuangalia njia nyingine ya kupata niahsati na kuachana na mradi huo.

“Kama nchi, tunafuatilia kwa dhati ushirikiano wa kinishati kabla ya kuzungumza juu ya kuongelea nishati mbadala,” anasema Ruth Nankabirwa, Waziri wa Nishati wa Uganda, wakati wa kilele cha mkutano wa saba wa kimataifa kuhusu mafuta na gesi uliofanyika Kampala, Uganda Septemba 2022.

Mafuta ambayo yanapita katika bomba hilo linalounganisha Uganda na Tanzania, yaligundulika mwaka 2006 katika Ziwa Albert, Uganda na kwamba ni moja ya maeneo yanayotajwa kuwa na kiasi kikubwa cha hifadhi ya mafuta duniani.

Zaidi ya miaka kumi baada ya kugundulika kwa kiasi kikubwa cha mafuta katika ziwa hilo, hakuna uzalishaji ulioanza kutokana na kuwepo kwa hofu



Rais Yoweri Kaguta Museveni wa Uganda

ya mradi kutumia muda mrefu na kiasi kikubwa cha uwekezaji kwa kuwa mafuta hayo yako kwenye kirefu cha ziwa, na mbali na eneo la pwani.

Baada ya mazungumzo ya miaka mingi, serikali za Uganda na Tanzania zilikamilisha makubaliano mwaka 2017 kwa ajili ya kujenga bomba la mafuta hayo ghafi hadi Tanga, Tanzania ili kusafirishwa kwenda nje ya Afrika kusafirishwa.

Endapo mradi huo utakamilika, inakadiriwa kuwa na uwezo wa kuzalisha mapipa 246,000 kila siku kwa ajili ya kusafirishwa hadi Bandari ya Tanga kwa ajili ya kupakiwa ndani ya meli za kimataifa.

Bomba hilo litasafirisha mafuta kutoka kituo cha kusukuma mafuta karibu na Hoima, Uganda, hadi kituo cha kuhifadhi mafuta kilicho Jiji la Tanga, kwenye pwani ya kaskazini mashariki mwa Tanzania.

Asilimia 80 ya bomba hilo linapitia nchini Tanzania. Ujenzi wake ulianza mnamo 2022, na linatarajiwa kukamilika mwaka 2025, ambapo tone la kwanza la mafuta hayo ghafi linatarajiwa kupakiwa ndani ya meli.

Mtazamo

Kuna ukakasi Sheria ya Habari

Na Mwandishi WETU

WADAU wa habari wameanza pilikapilika za uchechemuzi na uzengezi zinazolenga kuhamasisha kujumuishwa mapendekezo yao ili kuboresha mapendekezo ya Sheria ya Huduma ya Vyombo vya Habari ya 2016 yaliyowasilishwa bungeni na serikali.

Awali ilielekea kama vile kulikuwa na ufa miongoni mwa wadau hao wakati baadhi yao wakikubali marekebisho yaliyowasilishwa na serikali kama yaliyo kwa kuona kuwa nayo hiyo ilikuwa hatua chanya kwamba angalau wamesikilizwa na hatua imechukuliwa.

Wapo wadau waliona kuna haja ya kushinikiza mapendekezo yao mengi yaliyoachwa yafanyiwe kazi na kujumuishwa kwenye marekebisho yaliyo kwenye muswada wa marekebisho ya Sheria Mbalimbali.

Baada ya wadau kukutana katika vikao kadhaa ikiwemo mtandaoni, mwanga umeanza kujitokeza kwamba ipo haja ya mchakato wa marekebisho hayo ya sheria ya habari kupewa muda zaidi.

Hii ni kwa ajili ya kutoa nafasi ya wadau kutoa maelezo na ufafanuzi wa umuhimu wa kujumuishwa mapendekezo mengi ya marekebisho ya sheria hiyo ambayo hayakuzingatiwa katika marekebisho yaliyowasilishwa bungeni na serikali Februari, mwaka huu.

Katika moja ya vikao vya mtandaoni vilivyoendesha na Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF) ilionekana ni muhimu mapendekezo yote yazingatiwe ili kuepuka kupitisha marekebisho yaliyopwaya na kulazimika kufanya marekebisho mengine katika kipindi kifupi kijacho.

Kwa mtazamo wa wadau, ni bora kuchukua muda zaidi kupitia kwa makini suala hilo na kuwa na marekebisho mujarabu.

Haja kutoharakishwa mchakato wa marekebisho ya Sheria ya Huduma ya Habari ilisisitizwa pia na Mbunge wa



Waziri wa Habari, Nape Nnauye

Bunda, Esther Bulaya wakati akichangia katika mjadala wa Makadirio ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari bungeni, Dodoma - Mei 19, 2023.

Alimsihi waziri mwenye dhamana, Nape Nnauye, kuwa mchakato wa marekebisho hayo usiharakishwe, bali upewe muda zaidi.

Kinyume na matarajio ya awali ya wadau, mapendekezo ya marekebisho yaliyomo kwenye muswada uliowasilishwa bungeni na kusomwa kwa mara ya kwanza yameacha mapendekezo mengi ya wadau.

Kati ya mapendekezo 21 ya wadau ni tisa tu ambayo yameingizwa katika maboresho ya sheria hiyo yaliyowasilishwa bungeni na serikali.

Katika Sheria ya Habari yenye vifungu 66, masuala muhimu kama vile kutaka kuwepo na chombo kimoja badala ya kuwa vyombo viwili- Bodi ya Ithibati ya Wanahabari chini ya Baraza Huru la Habari hayakuzingatiwa.

Suala la kuondoa jinai kwa makosa ya utendaji ya kihabari na vilevile hukumu kuwa na ukomo na kuondolewa maneno mathalani "kifungo kisichopungua"... ni miongoni mwa masuala ambayo wadau wanachagiza kuwekwa sawa katika marekebisho hayo.

Habari Picha

Makao Makuu sasa rasmi Dodoma



Rais wa Samia Suluhu Hassan akiwa na Makamu wa Rais, Dkt. Philip Isidor Mpango (kulia) pamoja na Rais wa Zanzibar, Dkt. Hussein Ali Mwinyi mara baada ya kuingia ofisini kwake – Ikulu, Chamwino, mkoani Dodoma baada ya usinduzi wake rasmi Mei 20, 2023. (Picha zote na Ikulu).



Rais Samia Suluhu Hassan akikagua gwaride rasmi la ukaguzi lililoandaliwa na Jeshi la Polisi mara baada ya kuwasili katika Viwanja vya Ikulu ya Chamwino, Dodoma.

Rais Samia Suluhu Hassan akiwa kwenye picha ya pamoja na watumishi wa Ofisi Binafsi ya Rais (OBR) mara baada ya ufunguzi wa Jengo la Ikulu ya Chamwino, Dodoma.



Habari**Dkt. Mwinyi aamsha mageuzi****Na Mwandishi WETU,
Zanzibar**

ZANZIBAR inatarajiwa kuwa sehemu ya Tanzania yenye maendeleo makubwa kwa watu wake, endapo itaamua kukumbatia haki na ustawi wa demokrasia.

Inaeleza na wachambuzi wa “kukua na kukomaa kwa maendeleo” waliozungumza na Pambazuko na kubainisha kwamba hali ya utulivu, kuaminiana na kupendana kwa Wazanzibari, kutapaisha zaidi ustawi wa nchi hiyo iliyoungana na Tanganyika na kupatikana Tanzania, 1964.

Wachambuzi sita waliohojiwa wanasema kuwa kinachoonekana kukwamisha maendeleo makubwa ya Zanzibar ilikuwa ni kutoaminiana kwa makundi makubwa mawili ya watu wake; Wapemba na Waunguja.

Kwamba makundi hayo yakiamua kufanya kazi kwa pamoja na kuaminiana, Zanzibar inaweza kufikia maendeleo makubwa kwa kipindi kifupi.

Wachambuzi hao wanaeleza kwamba kutoaminiana kwa makundi hayo kunakomazwa na tofauti ya siasa; kati ya wafuasi wa vyama vya siasa; CCM na ACT-Wazalendo.

Hata hivyo, wachambuzi hao; Ismail Juma Hamad, Mwajuma Othman Machelo, Lucas Khamis Lusangija, Kulwa Kaminyonge, Jabir Hamis Lukhus na Dkt. Lenny Kasoga, wote wakiwa ni wasomi wa shahada mbili na tatu wamesema endapo uongozi wa sasa wa Zanzibar, utasimamia haki, kuna uwezekano mkubwa wa kuweka historia ya kufikia maendeleo makubwa katika kipindi kisichozidi miaka mitano,

Wachambuzi hao, wengi wakiwa wataalamu wa uchumi, siasa na maendeleo ya jamii, “wameweka wazi” kwamba Rais wa Zanzibar, Dkt. Hussein Ali Mwinyi ameonyesha dalili za kupigania maendeleo hayo kwa kuunganisha makundi mawili makubwa ya wanasiasa wa nchi yake.

**Rais Dkt. Mwinyi**

Wanaeleza kwamba ujenzi wa Zanzibar mpya kwa mnasaba wa mapendekezo ya “Kikosi Kazi” kilichokusanya maoni ya wadau kuhusu namna ya kuifikisha nchi kwenye amani ya kweli na demokrasia endelevu, unafufuka.

Mchambuzi mmoja, Dkt. Kasoga, ambaye ni mbobezi katika siasa uchumi, akiwa ni mhadhiri, anasema kwamba pamoja na kuwepo baadhi ya viongozi wastaafu wa Zanzibar kupinga mkakati wa maendeleo wa Dkt. Mwinyi, lakini “nia yake ni dhahiri” kuwa yuko makini “kuipaisha Zanzibar na kuwa – “kuna siku watumuelewa zaidi.”

Moja ya hatua ya kuimarisha demokrasia kwa Dkt. Mwinyi ni hatua muhimu ya kusonga mbele kwa suala la kuwakutanisha viongozi wa juu wa vyama vikuu vya siasa; Chama cha ACT-Wazalendo kuwasilisha majina ya wajumbe wa kuunda kamati ya kuchambua mapendekezo yaliyofikiwa kwenye mkutano wa siku tatu uliofanyika Septemba mwaka jana katiaka Hoteli ya Golden Tulip, Uwanja wa Ndege Zanzibar.

Chama hicho kikuu cha upinzani Zanzibar, kilikabidhi majina yake sita kwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi baada ya kukutana kwa majadiliano na wao kueleza utayari wao katika kukabiliana na hatua inayofuata baada ya Kikosi Kazi alichounda Rais Dkt. Mwinyi.

Dkt. Mwinyi aamsha mageuzi

Inatoka Uk. 10

Kikosi alichounda Dkt. Mwinyi kinahusika na masuala mahsusi yanayoihusu Zanzibar, baada ya kile kilichoundwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan kilichoongozwa na Prof. Rwekaza Mukandala.

Mazungumzo ya viongozi hao yalionyesha haja ya kukamilisha hatua ya mageuzi ya kisheria kama chachu ya kuimarisha haki, umoja na mshikamano katika nchi – ikiwa ni njia murua ya kufikia maendeleo ya kweli.

Viongozi wa ACT-Wazalendo waliahidi kuwa mstari wa mbele kuharakisha mazungumzo ya vyama vikuu vya kisiasa Zanzibar ambaye yatawezesha kutekelezwa kwa mapendekezo ya Kikosi Kazi cha Zanzibar kuhusu mageuzi ya kisiasa, kiutawala na masuala ya uchaguzi.

“Tunataka kuhakikisha kuwa vurugu na mauaji katika uchaguzi inakuwa ni jambo la historia kwa Zanzibar,” alisema Kiongozi Mkuu wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe kuhusu mazungumzo yao na Dkt. Mwinyi.

“Tunaamini tutakubaliana kwa mambo yote ya msingi,” anasema Othman Masoud Othman, ambaye pia ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, akiwakilisha chama hicho cha upinzani kwenye Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Katika hatua inayoonesha ukimya wa uongozi wa serikali katika kukabiliana ipasavyo na uvunjaji wa haki za binadamu uliotokea wakati wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2020, Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo Taifa, Juma Duni Haji alimkabidhi Dkt. Mwinyi ripoti inayotaja taarifa matukio mabaya ili kuchukuliwa hatua za kuelekeza nchi kwenye utawala wa sheria unaojali na kuzingatia misingi ya haki za binadamu.

Inaelezwa kuwa mmoja wa wajumbe wa ACT-Wazalendo katika kamati hiyo ni Othman, ingawa majina mnengina hayakuwekwa “ahdharani.” Kamati ya mazungumzo pamoja na Chama Cha

Mapinduzi (CCM), itazinduliwa na Rais Dkt. Mwinyi hivi karibuni.

Zanzibar imekuwa ikikumbwa na matukio mabaya wakati wa mchakato wa kila uchaguzi mkuu unaofanyika, tangu kuanza kwa mazingira ya vyaka vingi. Uchaguzi wa vyama vingi ulirejea Tanzania mwaka 1995.

Katika uchaguzi wa mwaka huu – 1995, hadi uchaguzi uliopita wa mwaka 2020, Zanzibar imekuwa ikikumbwa na matukio mabaya yanayokiuka haki za binadamu, ikiwamo watu kuuawa na kujeruhiwa na watu wanaoaminika kuwa askari wa vyombo vya ulinzi na usalama vya serikali.

Kuwepo kwa matukio hayo, kumekuwa kukisababisha kuvuruga mchakato wa kila uchaguzi na hata kutangazwa kwa matokeo.

Pamoja na kudaiwa kwamba CCM ndiyo ndiyo mnufaika mkubwa wa matukio hayo hadi kutangazwa kuwa mshindi wa kila uchaguzi, chama hicho tawala kimekuwa kikikataa kuhusika nayo.

Hatua hii ya vurugu wakati wa mchakato wa uchaguzi, imekuwa ikielezwa kuchochea manung’uniko kwamba demokrasia inabezwa kwa kutoendeshwa uchaguzi huru, wa haki na ulio huru utakaotoa matokeo ya kuaminika.

Kikao cha Rais Dkt. Mwinyi na viongozi wa ACT-Wazalendo, kimekuja wakati kukiwa na kimya cha muda mrefu tangu ulipomalizika mkutano ulioandaliwa na serikali kwa lengo la kutafuta maoni ya umma kuhusu mwelekeo wa mageuzi makubwa ya kisiasa, ikiwemo haja ya Zanzibar kupata Katiba inayokwenda na wakati baada ya ile ya mwaka 1984 iliyofanyiwa marekebisho makubwa mwaka 2010.

Kumekuwa na mashinikizo mbalimbali ya kutakiwa katiba mpya itakayoweka misingi na mifumo imara ya kuchagiza utawala bora, uwazi na uwajibikaji pamoja na katiba hiyo kuruhusu uhuru mpana wa kujieleza, kukusanyika na kushiriki shughuli za siasa.

Habari

Mkakati kupata asali tani 100,000

Na Amani NGONGOSEKE

SERIKALI imeweka mazingira ya kuwzesha wafugaji wa nyuki nchini Tanzania kuvuna zaidi ya tani 130,000 za asali kwa mwaka.

Mkakati huo wa serikali utahusisha ushirika wa wizara mbili; Wizara ya Maliasili na Utalii na Wizara ya Kilimo ambapo zitaanzishwa programu za matumizi ya makundi ya nyuki kwenye uchavushaji mimea ili kuongeza kiwango na ubora wa mazao nyuki yanayozalishwa.

Waziri wa Maliasili na Utalii, Mohamed Mchengerwa ameeleza hayo juzi-Jumamosi; Mei 21, wakati wa Kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Nyuki Duniani yaliyofanyika kitaifa katika Uwanja wa Bombadia, Singida na kuwataka wadau wa nyuki kutumia muda wao kujiendeleza ili kuelewa zaidi ufugaji huo.

Mchengerwa pia ametaka Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) na Mfuko wa Misitu kuhakikisha wanawezesha wananchi wanaopakana na maeneo ya hifadhi kwa kuwapa mafunzo bora ya ufugaji nyuki pamoja na mizinga ya kisasa. Pia kushirikiana na wadau mbalimbali kuhamasisha jamii kupanda na kuitunza miti katika maeneo yao.

Hivi sasa Tanzania, inakadiriwa kuzalisha tani 35,000 za asali, huku mkakati wa serikali ukipanga kufikisha hadi tani 138,000 – kiwango ambacho kinaelewa na wataalamu kwamba kinawezekana kufikiwa.

Mchengerwa ameupa jina mkakati huo kuwa ni “achia shoka, kamata mzinga” – ukibeba ujumbe kwamba tusikate miti, bali tuweje mizinga ya kuwahifadhi nyuki kwa kujihakikishia kipato.

Pia waziri huyo katika maadhimisho hayo amezindua Mwongozo wa Usimamizi wa Hifadhi za Nyuki, ambao unatoa fursa kwa wafugaji kuwa na fursa pana zaidi za kufaidika kwa ufugaji wa nyuki sambamba na mazo yake.

Akisoma hotuba yake amesema



Waziri Mohamed Mchengerwa

pamoja na uwepo wa maeneo makubwa yaliyohifadhiwa na yanayofaa kwa ajili ya kuzalisha mazao ya nyuki yenye viwango bora vado takwimu zinaonesha uzalishaji ni asilimia 23 ikilinganishwa na uwezo uliopo wa kuzalisha tani 138,000 kwa mwaka.

Mchengerwa amesema pamoja na serikali kuweka jitihada kubwa kwenye kulinda na kuhifadhi maliasili, bado katika kipindi cha hivi karibuni kumekuwa na kasi kubwa ya uharibifu wa maeneo yaliyohifadhiwa kutokana na shughuli mbalimbali za kibinadamu.

Mkoa wa Singida wenye uoto wa kipekee ujulikanao kwa jina maarufu kama Vichaka vya Itigi (Itigi Thicket) ambao unapatikana katika nchi mbili tu duniani, yaani Tanzania na Zambia, hivi karibuni umevurugwa na binadamu baada ya kukata miti hovyo.

Hali hiyo imesababisha sehemu kubwa ya ardhii iliyokuwa na uoto huu kubaki wazi na pia kumbainika kuwepo kwa mimea vamizi baada ya uoto huu ulipoondolewa. Kutokana na hali hiyo, waziri huyo ameelekeza TFS kuhakikisha kuwa maeneo yote yaliyobaki ambayo yana uoto huo yanatambuliwa na kuhifadhiwa kisheria, yalindwe.

Peoples... Power!



Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Aikael Mbowe (wa pili kulia) akiwa kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika Kata ya Munzeze, Jimbo la Buhigwe, Kigoma, Jumamosi – Mei 21, 2023. Chama hicho kiko katika operesheni maalum ya kudai katiba mpya iliyoanzia Kigoma. (Picha zote na mitandao ya Chadema).



Ngome ya wanawake wa Chadema wa Jimbo la Buhigwe wakiwa kwenye mkutano huo

Wanachama, wapenzi na mashabiki wa Chadema wakipunga mikono kuitimia salamu ya chama hicho; Peoples.. Power, katika mkutano huo.



Habari

Mtanzania awa gumzo Marekani

Na Mwandishi MAALUM

KIJANA wa Tanzania anayefanya kshughuli zake nje ya nchi hiyo, Joseph Rutakangwa, anaungana na vijana wengine duniani wenye ubunifu wa kutumia teknolojia kurahisisha kazi na matokeo yake kuonekana haraka, amekuza mtaji wake kufikia dola milioni nne.

Kiasi hicho cha fedha ni sawa na Shilingi za Tanzania bilioni 9.5. Fedha hizi zimetolewa na taasisi kadhaa ili kuongeza nguvu ya ubunifu kwa Mtanzania huyo.

Joseph ambaye kampuni yake Rwazi, imebuni mfumo ambao unawezesha kampuni, taasisi, mashirika na hata serikali kutumia teknolojia ya kisasa kukusanya, kuchakata na kusambaza taarifa za ujasusi wa masoko.

Tayari Rwazi imekuwa ikitajwa na taasisi kubwa za fedha na biashara kwamba ni miongoni mwa kampuni zinazochipukia kwa kukua kwa haraka na kuaminiwa kutokana na kuwa na mfumo wenye uhakika kupata na kupima matokeo.

Rwazi inatajwa kuwa miongoni mwa kampuni mujarab zinazimilikiwa na vijana kutoka nje ya Marekani na kwamba wameweza kuaminiwa kupewa kiasi kikubwa cha fedha ili kukuza ubunifu zaidi na kuongeza nguvu ya kusambaa zaidi kwa huduma zao.

Mfumo wa Kampuni ya Rwazi unatumia teknolojia rahisi na hauhitaji mtumiaji kuwa na ujuzi mkubwa wa mifumo ya kompyuta. Tayari taasisi na kampuni nchini Marekani zimeukubali ubunifu huo. Nchi zingine zinazotumia mfumo wa kampuni hizo ziko Afrika, Asia na Amerika Kusini.

Tangu kuanzishwa kwake, kampuni Rwazi inaongoza mabadiliko ya dhana katika mkabala wa ujasusi wa masoko, kwa kutumia mtandao wa vijana 50,000 dunia nzima katika kufuatilia bidhaa zinazouzwa na kuingia kwenye mzunguko wa biashara.



Joseph

Hadi sasa Rwazi ina wateja katika mataifa 60 yakiwamo ya Afrika, Asia, Marekani, Uingereza na Canada.

Mfumo wa kufanya kazi Kampuni ya Rwazi unaunganisha mitandao ya watumiaji, ambao unaipa kampuni hiyo taarifa za kijasusi kuhusu masoko katika huduma za kifedha na mawasiliano ya simu hadi huduma za afya.

Kampuni hiyo hutumia rasilimali watu kukusanya taarifa kupitia kwa watumiaji wa mtandaoni, ambao hulipwa kwa kushiriki maelezo kuhusu ununuzi wao.

Kampuni inapanga kutumia ufadhili huu ili kupanua wigo wake wa kibiashara na kuimarisha msimamo wake kama mhusika mkuu katika sekta ya ujasusi wa masoko.

Mzunguko wa mtaji wa dola milioni 4 unafanya jumla ya ufadhili wa Rwazi tangu kuanzishwa kwake 2018 kufikia dola milioni 7.8.

Kampuni hii inapanga kutumia ufadhili huu kuendesha mipango yake ya kimkakati ya upanuzi, kwa kuzingatia hasa kupanua ufikaji wake katika masoko yanayoibukia katika Afrika, Asia Kusini, na sehemu za Amerika Kusini.

Tangaza na Pambazuko

EWE mfanyabiashara na mtoa huduma, endapo unahitaji kuwafikia wateja wengi zaidi bila kujali mipaka ya eneo ulilopo, tangaza nasi

Pambazuko isaidie kupaisha na kupambazua huduma na biashara yako.



Kwa bei nafuu sana

0744 768 263 au Barua-
Pepe; info@pambazuko.tz

Habari Picha**Mahafali St. Joseph Cathedral**

Baadhi ya matukio katika picha kwenye mahafali ya 12 ya Shule ya Sekondari ya St. Joseph Cathedral, Dar es Salaam yaliyofanyika juzi – Jumamosi, Mei 21 ambapo jumla ya wanafunsi 230 walihitimu kidato cha sita.

Tuzibe pengo la 'falsafa' katika mitaala

Na Deusededith KAHANGWA

KUPITIA usimamizi wa Taasisi ya Elimu Tanzania, tayari Serikali ya Tanzania imechapisha "Rasimu ya Mitaala ya Elimu," tangu Mei 2023.

Rasimu hii ni sehemu ya mkakati wa mageuzi ya kimitaala. Je, mageuzi haya yanaongozwa na nadharia gani kuhusu utengenezaji wa mitaala? Najibu swali hili kwa ufupi.

Mitaala ya elimu katika nchi zote duniani, inagawanyika kwenye makundi makuu matatu.

Kwanza, kuna "Mtaala wa STEM," yaani "Mtaala wa Sayansi asilia, Teknolojia, Elimu ya uhandisi, na Hesabu." Yaani, "Science, Technology, Engineering and Mathematics."

Pili, kuna "Mtaala wa SHAPE," yaani "Mtaala wa Sayansi za jamii, Hulka za kibinadamu, Amali za Kisanaa, Pambanuzi za Kifalsafa na Elimu ya Uchumi." Yaani "Social sciences, Humanities, Arts, Philosophy and Economics."

Na tatu, kuna "Mtaala chotara," yaani mitaala ambao ni mseto wa "Mtaala wa SHAPE" na "Mtaala wa STEM," wenye ubora zaidi kwa sababu ya kuchukua mema na kuepuka madhaifu ya kila upande.

Huu ndio mkakati uliochukuliwa na Taasisi ya Elimu Tanzania katika zoezi la kurekebisha mfumo na mitaala ya elimu linaloendelea sasa hivi, ili hatimaye dira ya elimu ya kitaifa iweze kutimia.

Kwa kuzingatia nadharia hii, katika ngazi ya sekondari kutakuwa na michepuo kumi ambayo ni Sayansi ya Jamii, Kilimo, Biashara, Sayansi asilia, Sanaa, Lugha, Muziki, Michezo, Tehama na michepuo wa ufundi.

Bila kujali mwanafunzi anasoma mchepuo gani, kutakuwepo na masomo ya lazima kwa wote, yaani, hisabati, elimu ya biashara, kiingereza, na "historia ya Tanzania na maadili."

Somo la "Historia ya Tanzania na maadili" ni somo jipya tofauti na somo



Waziri wa Elimu Prof. Adolf Mkenda

la "historia" litakaloendele kufundishwa, kwa wanafunzi wa sayansi ya jamii, kama ilivyo sasa.

Hata hivyo, kwa kuangalia "umahiri" unaokusudiwa kupitia somo hili jipya, ni maoni yangu kwamba, halitatusaidia kufikia kiwango cha mageuzi ya kifikra kinachotakiwa. Badala yake, nafasi ya somo hili ikachukuliwe na somo jipya la "falsafa."

Yaani, tuandae na kufundisha "mtaala wa falsafa" wenye maudhui yaliyo katika sehemu kuu tatu.

Kwanza, ni "falsafa fafanuzi," yaani "descriptive philosophy," inayojumuisha ontolojia, saikolojia, kosmolojia, teodisia, epistemolojia, mantiki, semiolojia, na meriolojia.

Pili, ni "falsafa elekezi," yaani "normative philosophy," inayojumuisha tunu a kiakisiolojia, haki na majukumu ya kimaadili.

Na tatu, ni "falsafa matumizi," yaani "applied philosophy," inayohusu matumzi ya "falsafa fafanuzi" na "falsafa elekezi" katika sekta mbalimbali za maisha ya watu.

Hapa kuna falsafa ya uhuru, utumwa, ukoloni, umaskini, maendeleo, elimu, dini, afya, kilimo, ufugaji, uvuvi, uchumi, michezo, upendo, mapenzi, ndoa, mazingira, ujinsia, sheria, sayansi, historia, hesabu, biashara, na kadhalika. Linalowezekana leo lisingoje kesho. Tuamke.

Kenya**Lini Afrika itajisimamia?****Na Douglas MUTUA,
Nairobi**

HIVI Waafrika wana nia ya kusuluhisha matatizo yao wenyewe, bila kuhusisha viongozi wa mataifa ya nje – tena tajiri, au wao ni ‘domo-kaya’ tu?

Nimelazimika kulitafakari swali hili baada ya kumsikia Rais wa Kenya, William Ruto alipokuwa akiwasuta viongozi wa Afrika wanaosisitiza kwamba wakati umefika sasa kwa nchi za Afrika kuhakikisha zinalaliza matatizo yake yenyewe.

Ruto alisema pamoja na nia nzuri ya viongozi wa Afrika, je, wataweza kutatua changamoto zao wenyewe bila fedha ambazo “hawana.?”

Dkt. Ruto alilalamika hivyo akizungumza kuhusu mgogoro unaoendelea nchini Sudan, ambako majeshi ya pande mbili zinazokinzana kutaka madaraka, yanapigania kutwaa mamlaka.

Kando na kuwaambia majenerali wanaohusika ‘wakomeshe upuuzi huo’, alisema Waafrika hawawezi kuendelea kulisitiza kuhusu suluhu zao wenyewe ilhali juhudi zenyewe zinafadhiwa na wageni.

Alisema vita hivyo vinafanywa na Waafrika, vinaharibu miundo-mbinu ya Afrika, pamoja na kuwaua wanawake na watoto Waafrika.

Kauli ya Rais Ruto inaweza kuonekana nyepesi, lakini ni nzirto kwa kuwa imebeba mengi.

Ikuchukuliwa juujuu tu kauli hiyo, unaweza kudhani kwamba Dkt. Ruto ananua kuwafurahisha wageni waliompa kazi ya kuwapatanisha majenerali hao.

Tangu hapo huwezi kuung’ata mkono unayokulisha, hivyo lazima utumie akili. Hatujui kilichomsukuma kuyasema hayo hasa.

Hata hivyo, nadhani kauli yake ina ukweli fulani. Serikali za Afrika zimegeuka kuwa ombaomba hivi kwamba tatizo likizuka popote katika bara hili, mataifa wanachama wa Umoja wa Afrika (AU) hujikokota kulitatu, kwa kuwa



hayana fedha.

Waafrika wanatarajia mataifa tajiri yakiwamo ya Marekani, Ujerumani, Uingereza Ufaransa, Japan, China, Russia na mengine kutoa pesa, wao waalikwe kuhudhuria vikao tu.

Na ikitokea kwamba vikao vile havina posho, basi hakuna anayetaka kushiriki! Anachokitaka Mwafrika ni pesa za bure, apokee wala asitoe, zisipotoka humwoni pale! Hizo ni fikra za aina gani kwa mtu anayedai kutaka kujitawala?

Tangu hapo anayekulisha anakudhibiti; ukijulikana wewe mlafi, tumbo lako litashughulikiwa upesi, wanaokijua kinachotakiwa kufanya ili kujinufaisha waingie kazini kupanga mikakati ya kukurithi huku ukila na kucheua.

Nimeandika hapa awali kuwa mgogoro wa Sudan unahitaji kushughulikiwa na Waafrika wenyewe, na kufanya hivyo siyo kuhudhuria vikao na kupata posho za wafadhili tu.

Ni sharti Waafrika wagharimike, wawe na mfumo wa kushughulikia mizozo ya kisiasa na majanga ya kiasili yanayoweza kulikumba bara hili kama vile dhoruba, mafuriko, maporomoko ya ardhi na hata mlipuko wa maradhi.

Ni kutokana na tabia yao ya kuombaomba ambapo kote duniani viongozi wa Afrika huonekana kama kupe au watu wajanja wasiotaka kujituma katika kubadilisha hali yetu.



Mgunda aleta taharuki Simba

Kocha Juma Mgunda

MASHABIKI wa Simba wameingiwa na hofu kutokana na kutoonekana mazoezini kwa kocha msaidizi, Juma Mgunda, huku kukiwa na taarifa za chinichini huenda akatemwa na kurejea kwenye klabu yake ya zamani ya Coastal Union, lakini mwenyewe ameibuka na kutuliza presha hiyo.

Hofu ya mashabiki wa Simba ilitokana na kukosekana kwa kocha huyo kwenye mazoezi ya timu hiyo ilikuwa ikijiandaa kucheza na Ruvu Shooting na kuibuka uwanjani, pia kuonekana kwenye Uwanja wa Mkwakwani, jijini Tanga wakati Wagosi wa Kaya walipovaana na kuifunga Ihefu kwa bao 1-0.

Tangu Simba irejee mazoezini kujiandaa na mechi zilizosalia na kogea huyo hajaonekana mazoezini na kuzua presha kwa mashabiki waliohudhuria mazoezi hayo ya juzi na jana, huku ikielezwa taarifa yupo mbioni kupigwa chini ndizo zinazomnyima raha na kutoweka kambini, hata hivyo ameibuka na kufunguka kuwa, alikosekana kikosini kwa matatizo ya kifamilia na leo atakuwapo.

“Ni kweli sikuwepo mazoezini kwa sababu nilikuwa na mambo yangu ya kifamilia, lakini kesho nitakuwepo kuendelea na kazi, kwani mimi bado ni mfanyakazi wa Simba,” alisema Mgunda.

Licha ya Mgunda kusisitiza kwamba

bado anaendelea kuitumikia timu hiyo iliyopo nafasi ya pili ya Ligi Kuu kwa sasa nyuma ya mabingwa Yanga, lakini inaelezwa kitendo cha kuonekana kwenye mechi ya Coastal na Ihefu iliyopigwa wiki iliyopita iliwashtua zaidi mashabiki wa Msimbazi.

Ofisa Habari wa Coastal, Jonathan Tito alipoulizwa juu ya mipango ya kumrejsha Mgunda kikosini alijibu kuwa; “sisi tunaye kocha na kama mipango ya kutafuta kocha mpya basi sio kwasasa, kikubwa tunachokifikiria ni namna gani ya kumaliza mechi zetu mbili zilizobaki ili tushinde.

“Mgunda ni kati ya makocha wazuri wazawa, lakini suala la kusema anarejea au kuwepo kwenye mipango ya kumrejsha silifahamu kwa sasa. Sidhani kama lipo kwani halijajadiliwa popote ndani ya timu yetu, ninachofahamu hadi sasa ni kwamba Mgunda ni kocha wa Simba,” alisema Tito.

Mgunda alijiunga Simba, Septemba 7, mwaka jana na mechi ya kwanza kuiongoza timu hiyo ilikuwa kwenye mechi za awali za Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Big Bullets ya Malawi na kushinda ugenini kwa mabao 2-0, kisha kuiongoza kwenye Ligi Kuu dhidi ya Tanzania Prisons na kushinda 1-0.

Chogo la kutengeneza...



Jamii ya watu wa eneo la Mangbetu Kaskazini mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), tangu awali walikuwa na utamaduni wa “kutengeneza” vichwa vya watoto wao wachanga ili kuwa na umbo la mchongi kwa imani kwamba ubongo unatakiwa “kupumua” ili kuwa na uwezo mkubwa wa akili na kufikiri vyema. Hata hivyo, imani hiyo ilifika na kupotea kabisa miaka ya mwanzao ya 1950 baada ya kukomaa kwa dini za kigeni. Hii ni moja ya picha ambapo mtoto akiwa na mama yake – wote vichwa vyao “vimefinyangwa.

GAZETI hili huandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa). Pambazuko limesajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448.

